

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA SITA

KIKAO CHA TATU

29 AGOSTI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA SITA

KIKAO CHA TATU – TAREHE 29 AGOSTI, 2024

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI MKUU:

Maelezo ya Waziri Mkuu kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024 [*The Social Security Laws (Amendments) Bill, 2024*].

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024 [*The Social Security Laws (Amendments) Bill, 2024*].

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

40. MHESHIMIWA ALI JUMA MOHAMED (SHAURIMOYO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuharakisha malipo ya Wastaafu nchini.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

41. MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE WAITARA (TARIME VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya Kata ya Susuni Jimbo la Tarime Vijijini.

42. MHESHIMIWA ANNA RICHARD LUPEMBE (NSIMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Daraja la Mafunsi Kata ya Itenka - Nsimbo.

43. MHESHIMIWA BENARDETA KASABAGO MUSHASHU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali italipa madeni ya Wazabuni wanaotoa huduma za vyakula kwenye shule mbalimbali tangu mwaka 2023 hadi 2024.

44. MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, upi uwiano wa Mwalimu na Mwanafunzi Nchini.

WIZARA YA NISHATI:

45. MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENANI (NKASI KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Mkataba kati ya Tanzania na Wawekezaji wa Gesi Asilia wenye thamani zaidi ya Shilingi Trilioni 70 utaletwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa.

WIZARA YA UJENZI:

46. MHESHIMIWA PAULINE PHILIPO GEKUL (BABATI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa fidia Wananchi wa Babati waliopisha ujenzi wa barabara za mchepuko takriban miaka 4 iliyopita.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

47. MHESHIMIWA MUHARAMI SHABANI MKENGE (BAGAMOYO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itajenga Chuo cha VETA katika Halmashauri ya Bagamoyo kwa kuwa imekamilisha vigezo vyote muhimu.

WIZARA YA KILIMO:

48. MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO (BAHI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaanza ukarabati wa Skimu za Umwagiliaji zilizopo Kata ya Bahi.

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

49. MHESHIMIWA ABDUL YUSSUF MAALIM (AMANI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, tathmini ipoje juu ya utatuzi wa changamoto zitokanazo na Mashirikiano yaliyopo kati ya ZFF na TFF.

V. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024 [*The Social Security Laws (Amendments) Bill, 2024*].

DODOMA
29 AGOSTI, 2024

N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE